



















**MAAGIZO KWA WAPIGA KURA**

1. ILI KUPIGA KURA YA KUUNGA MKONO yoyote kati ya maswali yanayofuata, jaza duara dufu yenye alama ya NDIYO.
2. ILI KUPIGA KURA YA KUPINGA yoyote kati ya maswali yanayofuata, jaza duara dufu yenye alama ya LA.
3. KUPIGA KURA, JAZA DUARA DUFU HIVI:
4. Ukifanya kosa, rarua, au haribu karatasi hiyo ya kura, irudishe kwa afisa wa uchaguzi na kupewa kura nyingine. USIFUTE.

**1. UIDHINISHAJI WA BAJETI YA SHULE KWA MWAKA WA KALENDA WA 2022**

“Je, wapiga kura wa wilaya ya shule wataidhinisha bodi ya shule kutumia \$95,105,000 ambayo ni kiasi ambacho bodi ya shule imeamua kuwa ni muhimu katika kufuata mwaka wa kikalenda?”

Inakadiriwa kuwa bajeti hii iliyopendekezwa, ikiidhinishwa, itasababisha elimu kutumia \$17,069.13 kwa kila mwanafunzi sawa. Matumizi haya yanayotazamiwa kwa kila mwanafunzi ni 0.89% zaidi ya matumizi ya mwaka huu.”

NDIYO LA **2. MABADILIKO YA MKATABA YALIYOPENDEKEZWA ILI KUWAONGEZA WANACHAMA KWA BODI YA MAKAMISHNA WA UWANJA WA NDEGE**

“Je, Mkataba wa Jiji la Burlington, Vifungu vya 1949, Nambari 298, ilivyorekebisha, urekebisha zaidi ili kuongeza ukubwa wa bodi ya makamishna wa uwanja wa ndege hadi wanachama saba, ikijumuisha kuongeza mwakilishi kutoka Winooski na mwakilishi zaidi wa Burlington, kupitia marekebisha ya Mkataba wa Jiji \$120 na \$276?”

NDIYO LA **3. MABADILIKO YA MKATABA YALIYOPENDEKEZWA ILI KUDHIBITI MIFUMO YA KAWI YA JOTO**

“Je, Mkataba wa Jiji la Burlington, Vifungu vya 1949, Nambari 298, ilivyorekebisha, urekebisha zaidi ili kuruhusu Baraza la Jiji kudhibiti mifumo ya kawi ya joto katika majengo ya makazi na ya kibiashara, kupitia marekebisha ya Kitengo cha Mamlaka 48 ya Baraza la Jiji Yaliyoorodheshwa ili kuongeza mamlaka yafuatayo:

(67) Kudhibiti mifumo ya nguvu ya kawi ya joto katika majengo ya makazi na kibiashara, ikijumuisha kuchunguza athari ya kaboni au njia mbadala ya kulipa, kwa madhumuni ya kupunguza gesi inayoondolewa kwenye kivungulio katika jiji zima; hakuna tathmini ya athari ya kaboni au njia mbadala ya malipo itakayowekwa isipokuwa kama awali iliidhinishwa na wapiga kura wengi halali wa jiji husika wakipiga kura kwa swali katika mkutano wowote wa mwaka au wa jiji ulioitwa kwa madhumuni huo tu.?”

NDIYO LA **4. MABADILIKO YALIYOPENDEKEZWA YA MKATABA ILI KUDUMISHA KUPIGA KURA KWA CHAGUO ZENYE HADHI KWA MADIWANI WA JIJI**

“Je, Mkataba wa Jiji la Burlington, Vifungu vya 1949, Nambari 298, ilivyorekebisha, urekebisha zaidi ili kudumisha kupiga kura kwa chaguo zenye hadhi kwa uchaguzi wa madiwani wa jiji katika Jiji kwa kuanza na uchaguzi wa Machi 2022, kupitia marekebisha ya Mkataba wa Jiji wa § 5?”

NDIYO LA **5. MABADILIKO YA MKATABA YALIYOPENDEKEZWA ILI KUTOA ULINZI WA WAKAZI WA MAKAO KWA SABABU YA KUONDOLEWA BILA NJIA YA HAKI**

“Je, Mkataba wa Jiji la Burlington, Vifungu vya 1949, Nambari 298 vilivyorekebisha, virekebisha zaidi ili kuwapa Baraza la Jiji mamlaka ya kutoa kwa ulinzi wa hukumu kwa wakazi wa makao bila ‘njia ya haki’ kwa kuchukua na kuongeza kitengo kipya cha 48(66) ambacho

- kinatambua fasili fulani za njia ya haki;
- hakijumuishi kwa ‘njia ya haki’ kuisha muda kwa mapatano ya kukodisha kama msingi wa kipekee wa kumaliza ukodishaji, isipokuwa kwa mali fulani, chini ya utoaji wa umalizaji kama vile notisi ya kutosha;
- kinaweka vikwazo kwa ongezeko la kodi lisilo la kawaida ili kuzuia kuondolewa au kutoweka upya ukodishaji?”

NDIYO LA **6. KURUHUSU UUZAJI REJAREJA YA BANGI**

“Je, Jiji la Burlington litaruhusu uendeshaji wa wauzaji rejareja wa bangi ambao wamepewa leseni na Jimbo la Vermont chini ya Kifungu cha 164, kuanzia Oktoba 2022, mauzo kama hayo pia yanafuata hukumu au vikwazo vyovyote vya jiji ambavyo Jiji linaweza kutekeleza kinyume cha sheria?”

NDIYO LA **7. SWALI LA USHAURI WA HAKI YA HALI YA HEWA KATIKA UONDOAJI WA KABONI KWA JENGO**

“Je, wapiga kura wa Jiji la Burlington watashauri Baraza la Jiji na Mamlaka ya Meya, katika udhibiti wake wa mifumo ya kawi ya joto katika majengo ya wakazi na kibiashara, ili kuunda sera, mipango, na usaidizi unaolenga kutoa manufaa ya mpito wa kawi safi hadi kwa watu wa Burlington wenye mapato ya chini na kati, Weusi, Watu Asilia, na watu wenye rangi, na vinginevyo kwa watu wasiojiweza katika jumuiya?”

NDIYO LA **PIGA KURA KATIKA SEHEMU ZOTE ZA KURA**